TANGAZO LA SERIKALI NA. 630 la tarehe 19/10/2018

SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA YA 290

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO ZA MWAKA 2018

SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo za Mwaka 2018 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo;

''*Ada na Ushuru*" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni zitolewazo na Halmashauri;

''*Afisa Mwidhiniwa''* maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa

kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

''*Halmashauri*'' maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rombo;

"Kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri ;

"Kituo cha Mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kushusha abiria na mizigo;

"Madini ya ujenzi" maana yake ni Kokoto, Mawe, Moramu, Matofali, Mchanga, Chokaa, Pozzolana, Kifusi, Udongo Mfinyanzi, au kitu chochote kinachochimbwa katika Halmashauri kwa shughuli za ujenzi ;

"Maegesho'' maana yake ni sehemu maalum iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda ;

"Masoko" maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza na kununua bidhaa ;

''Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au mtumishi wa umma atakayekuwa anatekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"*Mkusanya ushuru*" maana yake ni mtu binafsi, kampuni, kikundi au taasisi yeyote ambayo itaingia mkataba na Halmashauri kwa ajili ya kukusanya ada au ushuru;

"Mnada" maana yake ni sehemu iliyotengwa

na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa kwa siku maalum;

SEHEMU YA PILI
KUTOZA NA KUKUSANYA ADA NA USHURU MBALIMBALI.

Ada na Ushuru mbalilmbali

4. (1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyooneshwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(a) Ada itozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi italipwa kabla ya huduma kutolewa

(b) Ushuru utozwao chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa saa au siku au kabla ya kupata huduma au wakati wa kupata huduma

(2) Huduma zitakazotozwa Ada na Ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni;-

(a) Kibali cha ujenzi

(b) Upimaji wa kiwanja

(c) Vyombo vya usafiri vinavyoingia katika magulio, stendi, masoko na minada

(d) Ukaguzi wa nyama

(e) Mazao mchanganyiko

(f) Mazao ya misitu

(g) Kumbi za Halmashauri

(h) Kukodi magari ya mitambo na mashine ya Halmashauri

(i) Vibanda na vizimba vinavyomilikiwa na Halmashauri

(j) Ukaguzi wa afya

(k) Kusajili vikundi

(l) Madini ya ujenzi

(m) Vyoo vinavyomilikiwa na Halmashauri

(n) Mazao ya bahari

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. (1) Malipo yote ya Ada yatafanyika kwa miezi mitatu au sita au kwa mwaka.

(2) Malipo yote ya Ushuru yatafanyika kwa saa au siku.

(3) Malipo ya Ada au Ushuru unaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kama kielelezo cha malipo.

(4) Ni wajibu wa mtu yeyote atakayelipa Ada au Ushuru kudai na kuhakikisha anapewa stakabadhi halali kwa malipo anayotoa.

(5) Malipo yote ya Ada na Ushuru yanayopaswa kulipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, yatalipwa kabla ya huduma kutolewa na Halmashauri.

(6) Bila kuathiri Masharti ya kifungu cha 5(1) (2) mlipaji wa Ada au Ushuru anaweza kuingia katika makubaliano na Halmashauri kuhusu muda wa kulipa Ada au Ushuru.

Mkusanya ada na Ushuru

6. (1) Halmashauri inaweza kuingia mkataba na Mkusanya Ushuru kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

(2) Pale ambapo Halmashauri itaona inafaa kutumia Mkusanya Ada na Ushuru kwa madhumuni ya kurahisisha ukusanyaji na kuepuka gharama za ukusanyaji, itafanya tathimini ya kina juu ya chanzo hicho.

Uwezo wa kumuita mlipa ada au ushuru

7. Mkurugenzi anaweza kumuita mlipa Ada au Ushuru yeyote afike mbele yake au mbele ya Afisa mwidhiniwa kwa muda unaofaa na kutoa maelezo yanayohitajika kuhusiana na malipo ya Ada au Ushuru.

Uwezo waAfisa mwidhiniwa

8. Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA TATU
MAKOSA NA ADHABU

Makosa

9. Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi kwa mtu yeyote:-

(a) kukaidi au kushindwa au kudharau kulipa Ada au Ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kukusanya au kujaribu kukusanya Ada na Ushuru bila ya kuruhusiwa na Halmashauri kwa maadishi au kutoza kiwango cha juu

zaidi ya kile kilichowekwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

(c) kushindwa kuleta taarifa zozote Halmashauri ımbazo
zinahitajika kuthibitisha ulipaji wake wa Ada ıu Ushuru ndani
ya muda alioelekezwa na Halmashauri;

(d) kumzuia Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Halmashauri kutekeleza kazi chini ya Sheria Ndogo hizi;

Adhabu

10. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000) na isiyozidi shilingi Milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miaka miwili (2) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo;

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi kwa hiari yake mwenyewe na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa, kama ilivyoelekezwa katika jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi;

GN Na. 371 ya tarehe 3/10/2014

12. Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya Rombo za mwaka 2014 zinafutwa.

JEDWALI LA KWANZA

(Limetungwa chini ya Kifungu cha 4(1))
SEHEMU YA KWANZA

Ada ya Kibali cha ujenzi.

	Ukubwa wa kiwanja	Kiasi cha ada
1.	Nyumba za makazi kwenye Kiwanja kikubwa (Low Density)	40,000/=
2.	Nyumba za makazi kwenye Kiwanja cha kati (Medium density)	30,000/=
3.	Nyumba za makazi kwenye kiwanja kidogo (High density)	20,000/=
4.	Viwanda, mahoteli na nyumba za kulala wageni bila kujali ukubwa wa kiwanja.	500/= kwa kila mita moja ya mraba
5.	Jengo la gorofa kwa kila floor/gorofa bila kujali ukubwa wa kiwanja	500/= kwa kila mita moja ya mraba
6.	Majengo mengine (mfano maduka)	500/= kwa kila mita moja ya mraba
7.	Kibali cha kuweka minara ya simu	500,000/= kwa mnara

SEHEMU YA PILI

Ada ya upimaji wa kiwanja

1.	Ukaguzi wa ramani	5,000/= kwa kila ramani
2.	Kiwanja cha Makazi	2,000/= kwa Mita moja ya Mraba
3.	Kiwanja cha Biashara	3,000/=kwa Mita moja ya Mraba

SEHEMU YA TATU

Ushuru wa vyombo vya usafiri vinavyoingia katika magulio, stendi, masoko na minada ya Halmashauri.

Na.	Aina na uwezo wa gari	Kiasi
1.	Gari la zaidi ya abiria 39.	2,000 kwa siku
2.	Gari la abiria 20-39	1,500/= kwa siku
3.	Gari dogo la abiria chini ya 20	1,000/=kwa siku
4.	Teksi	500/= kwa siku
5.	Magari binafsi yasiyo ya biashara	500/= kwa siku
6.	Gari dogo la mizigo [pick up/ lorry chini ya tani 7]	2,000/= kwa siku
7.	Gari kubwa zaidi ya tani 7	2,500/= kwa siku
8.	Piki piki (boda boda)	200/= kwa siku
9.	Mikoteni ya aina yote	200/= kwa siku
10.	Bajaji	500/= kwa siku
11.	Noah	24,000/=kwa mwezi

SEHEMU YA NNE

Ushuru wa ukaguzi wa nyama mnadani na kwenye mabucha

Na.	Aina ya mfugo	kiasi
1.	Ng'ombe	5,000/= kwa ng'ombe mmoja
2.	Mbuzi	2,000/= kwa mbuzi mmoja
3.	Kondoo	2,000/= kwa kondoo mmoja
4.	Nguruwe	3,000/= kwa nguruwe mmoja

SEHEMU YA TANO

Ada ya ushuru wa Mazao ya Kilimo

Na.	Aina ya zao	Kiasi
1.	Kahawa	3% ya bei ya kununulia
2.	Ndizi	3% ya bei ya kununulia
3.	Viazi mviringo	3% ya bei ya kununulia
4.	Viazi vitamu	3% ya bei ya kununulia
5.	Magimbi	3% ya bei ya kununulia
6.	Maharage/Karanga/Choroko/Mchele/Kunde	3% ya bei ya kununulia
7.	Mahindi/Alizeti/Uwele/Mtama/Mpunga/Mihogo	3% ya bei ya kununulia
8.	Vitunguu maji/Vitunguu saumu/ Matunda/ Karoti/ Kabichi/Nyanya	3% ya bei ya kununulia

SEHEMU YA SITA

Ada ya mazao ya misitu.

Na.	Aina ya zao	Kiasi
1.	Mbao	1pc Tsh 200/=
2.	Mabanzi	1 pc Tsh 100/=
3.	Nguzo	1 pc Tsh 100/=
4.	Kibali cha kukata/kuvuna mti	1,000/= kwa mti mmoja
5.	Kuni/Lorry kuanzia Ton ½ - 1	Tsh 5000/=
6.	Kuni/Lorry kuanzia Ton 1 ½ - 3 ½	Tsh 10,000/=
7.	Kuni/Lorry kuanzia Ton 4 – 7	Tsh 15,000/=
8.	Kuni/Lorry kuanzia Ton 7 ½ - 10	Tsh 20,000/=
9.	Kuni/Lorry kuanzia Ton 10 ½ - na kuendelea	Tsh 50,000/=

SEHEMU YA SABA

Ada ya kukodi kumbi za Halmashauri.

Na.		Kiasi
1.	Kukodi ukumbi wa Halmashauri kwa ajili ya Mikutano/ Vikao.	100,000/= kwa siku

SEHEMU YA NANE

Ada ya kukodi magari ya mitambo na mashine za Halmashauri.

Na.		Kiasi
1.	Ada ya kukodi gari	Kama itakavyoamuliwa na Halmashauri kutegemeana na gharama za umbali, gharama za mafuta na matumizi ya mkodishaji na muda wa gari kukodishwa.
2.	Ada ya kukodi mashine au mtambo	Kama itakavyoamuliwa na Halmashauri kutegemeana na gharama na aina ya mashine na muda wa mkodishaji kutumia.

SEHEMU YA TISA

Ada ya upangishaji wa eneo la vibanda vya Vituo vya mabasi, Sokoni na Garden Square na Vizimba vya Sokoni.

Na.		Kiasi
1.	Ada ya upangishaji wa eneo la vibanda vya Kituo cha mabasi (Mkuu na Holili) Sokoni (Mkuu, Holili, Usseri na Tarakea) na Garden Square Mkuu.	Tsh 15,000/= kwa mwezi
2.	Ada ya kukodi kizimba sokoni	10,000/= kwa mwezi

SEHEMU YA KUMI

Ada ya Ukaguzi wa Afya

Na.	SAFU YA KWANZA	SAFU YA PILI: kiasi cha ushuru
1.	Nyumba za starehe, baa, hoteli, migahawa na vilabu vya pombe za kienyeji	5,000/= kwa kila baada ya miezi sita
2.	Nyumba za kulala wageni	5,000/= kwa kila baada ya miezi sita
3.	Maduka ya bidhaa	2,000/= kwa kila baada ya miezi sita
4.	Nyumba za kutengeneza na kuuzia vyakula na nyama choma	3,000/= kwa kila baada ya miezi sita
5.	Ukaguzi wa maombi ya kufungua biashara	5,000/=kwa kila baada ya miezi sita
6.	Ukaguzi wa viwanda vikubwa	100,000/= kwa kila baada ya miezi sita
7.	Ukaguzi wa viwanda vya kati	50,000/= kwa kila baada ya miezi sita

8.	Ukaguzi wa viwanda vidogo	20,000/= kwa kila baada ya miezi sita
9	Mama ntilie na magenge ya aina yote	5,000/= kwa kila baada ya miezi sita
10.	Ukaguzi wa karakana	50,000/= kwa kila baada ya miezi sita
11.	Masuala ambayo hayajatajwa na yanahitaji ukaguzi	3,000/= kwa kila baada ya miezi sita

SEHEMU YA KUMI NA MOJA

Ada ya kusajili vikundi ndani ya Halmashauri

Na.	Aina ya kikundi	kiasi cha Ada
1.	Vikundi vya aina yoyote.	10,000/=

SEHEMU YA KUMI NA MBILI

Ushuru wa madini ya Ujenzi

1.	Ushuru wa Pozollana	3,000/= kwa tani
2.	Ushuru wa Matofali ya kuchonga	5,000/= kwa lori
3.	Ushuru wa Matofali ya kufyatua (Blocks)	50,000/= kwa mwaka
4.	Ushuru wa Mchanga	5,000/= kwa lori
5.	Ushuru wa kokoto	5,000/= kwa lori
6.	Ushuru wa Moramu	5,000/= kwa lori
7.	Udongo mfinyazi	5,000/=kwa lori

SEHEMU YA KUMI NA TATU

Ushuru wa Vyoo

Na.	AINA YA JENGO	USHURU
1.	Vyoo vya stendi	300/ = kwa kila mtu
2.	Vyoo vya sokoni	300/= kwa kila mtu
3.	Huduma ya Bafu	500/= kwa kila mtu

SEHEMU YA KUMI NA NNE

Ushuru wa Mazao ya bahari

Sangara,sato,Dagaa,Mabondo na samaki wengine	Tshs. 500/= kwa tenga

JEDWALI LA PILI

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

(Chini ya kifungu cha 11)

Mimi ……wa S.L.P…….ninayefanya biashara katika eneo la……..lilolopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo. Nakiri kuwa leo tarehe……..nilikiuka kifungu cha …….cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo za mwaka 2018.

Kwa hiyo Kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa kiasi cha ushuru ninodaiwa pamoja na faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 11 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini: ……

Mbele yangu……..(Jina)

Saini……

Wadhifa……

Tangazo la Serikali Na. 630 (Linaendelea.)

Nembo ya Halmashauri imegongwa katika Sheria Ndogo hizo kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Rombo uliofanyika mnamo Tarehe 31/7/2017 na Nembo iliyogongwa mbele ya:-

MAGRETH L. JOHN
Mkurugenzi
Halmashauri ya Wilaya ya
Rombo

L.S

EVARIST A. SILAYO,
Mwenyekiti,
Halmashauri ya Wilaya ya
Rombo

NAKUBALI,

Dodoma,
14 Aprili, 2018

SELEMANI S.JAFO (MB)
Waziri wa Nchi-or Tamisemi